# SautiElimu

hakielimu

Toleo la 2
2002/3

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org




## Je, Unaielewaje Maana ya Elimu Bora?

### Kutoka kwa Mhariri

**Na Rakesh Rajani,** Mkurugenzi Mtendaji, HakiElimu

Sote tunakubali elimu ni ufunguo wa maisha lakini je, inatosha kuwajaza wanafunzi madarasani bila kujali ubora wa elimu? Kwani maana ya elimu bora ni nini?

Sisi tunaamini kuwa kila mtoto Tanzania-bila kubaguliwa ana haki ya kusoma katika shule bora.

Shule bora ni ile inayomjali mtoto, yenye mwamko wa kujifunza, ambapo kila mtoto anashiriki kikamilifu ndani na nje ya darasa. Shule nzuri ni ile ambayo inamkaribisha na kumthamini kila mtoto, kumpa moyo wa kuwa wazi, kuuliza maswali, kufikiri, kuwa mdadisi na mbunifu.

Shule nzuri ni ile yenye walimu wanaojali, wenye uwezo na wanaojituma, wenye kutafakari na kuendelea kujifunza, wanaovutiwa na mazingira bora ya kazi na kuwajibika katika kazi zao. Ni sehemu ambayo uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi unadhihirishwa kwa kuaminiana na kuheshimiana.

Shule nzuri ni mahali pa usalama na heshima kwa watoto wote. Ni sehemu ambayo watoto hawapigwi au kuadhibiwa kwa njia zinazowadhalilisha. Ni sehemu ambapo watoto wote, hasa watoto wa kike na wenye ulemavu, hawabaguliwi, kuonewa na wala kunyanyaswa na mtu yeyote.

Shule nzuri ni ile inayoongozwa vyema kwa njia za kidemokrasia, ni pale ambapo utawala ni shirikishi na unaihusisha jamii kikamilifu. Ni sehemu ambapo watoto wana sauti katika utawala wa shule. Ni mahali ambapo rasilimali zinatumika vizuri kwa uwazi na uwajibikaji.

Shule nzuri ni muhimu kwa uraia bora; inahakikisha kwamba watoto wana ujuzi, ubunifu, msukumo na ari ya maendeleo yao wenyewe na maendeleo ya kidemokrasia kwa taifa zima.

Toleo hili la SautiElimu linatoa baadhi ya maoni kuhusu elimu bora. Lakini sasa tunataka kukusikiliza wewe. Je, unaielewaje maana ya elimu bora? Tuambie!

## Baraza la Wanafunzi Kujadili Maendeleo ya Shule

**Na James Mikenze,** Ukerewe

Shule ya  Msingi Nkilizya, iliyopo wilayani Ukerewe, imeunda Baraza la Wanafunzi ili kujadili shughuli mbalimbali za maendeleo shuleni hapo.


Baraza hilo lililochaguliwa kidemokrasia na wanafunzi wenyewe lina kazi ya kujadili ufundishaji wa walimu pamoja na mahudhurio yao darasani.

Utoro wa wanafunzi ni moja ya mambo ambayo yatafuatiliwa kwa kina na Baraza hilo na kutafutiwa suluhu kwa njia ya mijadala ya wanafunzi, walimu, wazazi na jamii inayoizunguka shule. Idadi ya wanafunzi shuleni hapo ni 760, wa kike 390 na wa kiume ni 370.

Muundo wa kamati ya shule unaozingatia Waraka wa Elimu namba 14 wa Juni 2002 umeanza kutekelezwa shuleni hapo. Waraka huo unahimiza kuwepo kwa wawakilishi wawili wa wanafunzi, mmoja wa kiume na mwingine wa kike, katika kamati ya shule.

Ushirikiano mzuri kati ya shule na jamii ya Nkilizya ni mfano wa kuigwa kwani unatoa fursa kwa wadau wote kushiriki katika mkakati wa kuleta maendeleo ya elimu nchini.

Timu ya SautiElimu inawapongeza wana Nkilizya!




## Wanafunzi Waanza Kushiriki Kamati ya Shule

**Na Mzee Said Omari,** Mjumbe Kamati ya Shule, Tandika Mabatini

Mwezi Juni mwaka 2002, nilikuwa nikipita katika maeneo ya Upanga jijini Dar es Salaam. Nia ya kuvinjari katika maeneo hayo ilikuwa ni kutafuta ofisi ya HakiElimu. Awali nilipata maelezo ambayo si sahihi kwamba HakiElimu ilikuwa ikitoa msaada wa kifedha kusomesha wanafunzi.

Nilifanikiwa kufika katika ofisi za HakiElimu ambapo nilipokelewa na kupewa maelezo ya kina kuhusu shughuli za shirika hilo na kwamba halihusiki kutoa misaada ya kifedha.  Hata hivyo, nilivutiwa na habari ambayo ilikuwa ngeni masikioni mwangu kuwa shirika hili linahimiza ushiriki wa umma katika utawala wa elimu.

Nikiwa kama mmoja wa wazazi na mjumbe wa kamati ya shule yangu nilipata hamu ya kudadisi zaidi ili niweze kuelewa kwa undani kile nilichokuwa nikielezwa. Nilipata maelezo mengi na moja ambalo lilinigusa zaidi ni ule mfumo wa kamati ya shule. Kamwe sikujua kama wanafunzi nao wanatakiwa kushiriki katika kamati ya shule!
Pamoja na maelezo hayo nilipata pia vipeperushi ambavyo vilieleza shughuli za HakiElimu. Nilikwenda katika ofisi ya HakiElimu nikiwa na matarajio tofauti lakini niliondoka na mawazo makubwa ambayo yamesaidia kutoa mtazamo mpya katika uongozi shuleni kwetu.

Kwa bahati nzuri niliweza kujadiliana na wazazi na wajumbe wenzangu katika kamati ya shule kwa kutumia maelezo na vipeperushi vya HakiElimu. Hiyo imetuwezesha kuwa na wajumbe ambao ni wawakilishi wa wanafunzi, mmoja wa kike na mwingine wa kiume, katika kamati ya shule yetu.

Pia tumeanzisha mikakati ya kuzishawishi shule nyingine katika kata yetu kuhakikisha kuwa zinafuata mwongozo wa serikali kushirikisha wanafunzi katika kamati za shule. Mchango wa wanafunzi ni muhimu katika kuboresha Elimu nchini!

## Kauli ya Mzazi kuhusu Elimu Bora

**Na Joseph Kulangwa,** Dar es Salaam

Kuna matatizo mbalimbali yanayoifanya elimu nchini idumae. Hayo ni yale yanayomzuia mwalimu kuhamisha maarifa kwenda kwa mwanafunzi. Kwa upande wa pili mwanafunzi naye hushindwa kutoa mrejesho kwa mwalimu wake na hata kupokea maarifa hayo.

Matatizo yanayozumgumziwa kila mara ni kama vile watoto kusomea nje ya madarasa, ukosefu wa madawati, na upungufu au ukosefu wa vifaa vya kufundishia.



Yawezekana vitu hivyo vyote vikawepo katika shule lakini kusiwe na walimu wa kutosha wala wenye ujuzi unaostahili. Vilevile walimu wanaweza kuwa wengi lakini elimu inayotolewa ikawa si bora. Twaweza kuuliza, inawezekanaje kuwa na vifaa na walimu wa kutosha na bado elimu ikawa duni?

Ili elimu iwe bora nchini, ipo haja ya kujadiliana na wadau wote jinsi ya kumaliza matatizo yanayomkabili kila mdau. Mathalan, maslahi ya walimu yakiboreshwa yatampa motisha mwalimu aweze kufundisha kwa bidii na kuwa makini katika kazi yake. Hii iende sambamba na mafunzo ya mara kwa mara kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Lakini lililo zito zaidi ili elimu iwe bora ni uhusiano kati ya mwanafunzi na mwalimu wake darasani na nje ya darasa. Uhusiano mzuri utamfanya mwanafunzi kuwa jasiri wa kuweza kuelewa, kutafakari na kutoa mrejesho wa mafundisho ya mwalimu wake. Utampa mwanafunzi uwezo wa kuwa raia bora anayetambua haki zake na kufuata misingi ya haki za binadamu.

## Mitaala Shule za Msingi iwe ya Vitendo

**Na Huba Msonga,** Shule ya Msingi Mzase, Mpwapwa

Elimu inayotolewa kwa sasa katika shule za msingi imeegemea zaidi upande wa nadharia. Hiyo ni moja ya sababu inayochangia kushuka kwa elimu kwani kamwe haimjengi mwanafunzi kuwa mbunifu. Elimu bora ni ile inayomwezesha mtoto kukabiliana na maisha pindi atakapo maliza shule ya msingi.

Mitaala ya elimu ya msingi inatakiwa  ibadilishwe ili kuwe na masomo ya useremala, ushonaji, ufundi wa umeme na magari, sanaa za mikono na mengineyo yatakayomwezesha mwanafunzi kujiajiri baada ya kumaliza shule ya msingi.

Elimu bora pia itapatikana kwa kuzingatia kuwepo kwa vifaa vya kufundishia na walimu wa kutosha wenye uwezo wa kufundisha. Mazingira mazuri ya shule ni moja ya vigezo lakini ni muhimu pia kuzingatia mahitaji ya wanafunzi. Mathalan, kuwapatia chakula shuleni na kutoa kipaumbele kwa michezo ili kukuza vipaji vyao.



Ukurasa wa 1

SautiElimu

hakielimu

Toleo la 2
2002/3
ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

# Matukio katika Elimu

Matukio makuu mawili katika sekta ya Elimu yalifanyika jijini Dar es Salaam.

Tukio la kwanza ni Mkutano wa Wabunge wa Afrika wanaoshughulikia Elimu (FAPED) ambao ulifanyika kuanzia Novemba 27 hadi Desemba 2, 2002.

FAPED ina lenga kuwashirikisha wabunge wa Afrika katika masuala yahusuyo Elimu kama vile kufuta ujinga, kuondoa umaskini, kuhimiza elimu kwa wasichana na wanawake na kupambana na UKIMWI. FAPED pia inahimiza wabunge kutafuta vyanzo zaidi vya mapato.

FAPED ni chombo kipya na mkutano wa Dar es Salaam ulikamilisha ufafanuzi wa vipengele vinavyoeleza majukumu na madhumuni yake.

Tukio la pili lilikuwa Mkutano wa Mawaziri wa Elimu barani Afrika (MINEDAF VIII).
Mkutano huo ulifanyika Dar es Salaam kuanzia Desemba 2 hadi 6 2002. Mawaziri wote wa Elimu barani Afrika walialikwa kuhudhuria.

Mada ya mkutano huo ilikuwa ni "Kukabili changamoto za elimu Afrika kutoka kudhamiria kwenda kwenye vitendo". Mazungumzo yalizingatia suala la Elimu kwa Wote, (EFA) katika nchi zote za Afrika kwa kipindi cha miaka 15 ijayo.



Nini matarajio ya elimu nchini baada ya mkutano huo?
Kwa vile tukio hili linafanyika Tanzania, suala la mfumo wa elimu nchini litatiliwa mkazo. Kuwepo kwa idadi kubwa ya wajumbe kutoka nchi nyingine za Afrika, kutatoa fursa ya kubadilishana uzoefu katika masuala ya elimu.

Mashirika ya kijamii yatahusishwaje?
Mwezi Septemba 2002 Asasi Zisizo za Kiserikali na Mashirika ya Kijamii zaidi ya 200 barani Afrika yalikutana na kujadili jinsi ya kuyapa nguvu matokeo ya mkutano wa MINEDAF. Wawakilishi kutoka hapa nchini pia walishiriki. Makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano huo yaliandikwa na ripoti ilisomwa wakati wa mkutano wa MINEDAF. Ripoti hiyo inaelezea mtazamo wa Mashirika ya Kijamii kuelekea Elimu kwa Wote (EFA).

Wakati wa mkutano huo, Mashirika ya Kijamii pia yalipata nafasi ya kutangaza shughuli zao na kufanya maonesho ya vitu wanavyozalisha.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na HakiElimu au andika kwa:

UNESCO National Commission
SLP 20384
Dar es Salaam
Tovuti: www.minedaf.org

# HakiElimu Yazindua Marafiki wa Elimu

Mwezi Desemba 2002, HakiElimu itazindua rasmi harakati zijulikanazo kama *Marafiki wa Elimu.* Madhumuni ya harakati hizo ni kuwawezesha wakereketwa wa elimu nchini kushiriki pamoja kutoa na kujadili maoni ili kuboresha elimu nchini Tanzania.

Washiriki wa harakati hizi ni watu wote wakiwemo watoto, vijana, wazee, watu wenye ulemavu, watu wenye kipato duni, na jamii kwa ujumla. Wengine ni vikundi, mashirika na taasisi mbalimbali zilizo tayari kushiriki katika kuboresha elimu nchini.


Wanaharakati wanategemewa kuwa wabunifu na kuungana na wenzao ili kuibua masuala muhimu kwa niaba ya jamii wanamoishi au wanamofanyia kazi. Pia watachangia;
- kukuza na kutekeleza sera ya elimu;
- kushiriki katika kampeni mbalimbali za elimu
- kupeana taarifa muhimu za elimu na kubadilishana uzoefu na
- kutoa msukumo wa pamoja wa mabadiliko katika elimu hapa nchini.




Maelezo ya kina kuhusu *Marafiki wa Elimu* yanapatikana katika machapisho yanayotolewa na HakiElimu kama vile kipeperushi na kijitabu cha *Marafiki wa Elimu* kwa ajili ya wanaharakati, na kupitia: rafiki@hakielimu.org.

Hii ni nafasi yako ya kushiriki katika kutoa maoni na kujifunza kutoka kwa wengine!

# Barua kwa SautiElimu



Mhariri SautiElimu, Nimebahatika kusoma moja ya machapisho yenu, SautiElimu. Nimefurahishwa na mada zilizojitokeza katika jarida hilo pamoja na picha. Nawapongeza kwa kazi yenu ya kuichochea jamii ili iweze kujadili na hatimaye kuboresha elimu nchini.

Hata hivyo, nimesikitishwa na picha ambayo kwa mtazamo wangu inaelekea kuwa ni kamati ya shule mojawapo nchini. Picha ya kamati hiyo ina mjumbe mmoja tu mwanamke! Je, huo ndio muundo wa kamati ya shule?

Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 rekebisho no. 14 la mwaka 1995, linaeleza kwamba wajumbe wa kamati ya shule ni lazima wawe wa jinsi tofauti. Nashauri mtumie picha ambazo zitawaongoza wananchi badala ya kuwachanganya.

**Anna Maua**
Dar es Salaam

•••

Mhariri SautiElimu, Napenda kutoa maoni yangu kuhusu elimu bora. Kwa ufupi, ni ile ambayo inamjali kila mtoto, awe tajiri, maskini, mwenye ulemavu au wa jinsi yoyote.

Kwa bahati mbaya baadhi ya wazazi na walezi nchini hawapendi kuwapeleka shule watoto wenye ulemavu. Anapozaliwa mtoto mwenye ulemavu hunyanyaswa na kuonekana kwamba hana faida katika familia.

Ili kupata idadi kubwa ya watoto wenye ulemavu wanaojiunga na shule, nashauri serikali na jamii kuweka vivutio maalumu shuleni kama vile vifaa vitakavyowasaidia kulingana na maumbile yao.

Vile vile kuwe na mpango maalumu wa kuwahamasisha wazazi wa watoto wenye ulemavu kuwapeleka shule. Wanaweza kuhamasishwa kupitia vyombo vya habari na hata taasisi za kijamii.

**Dotto Ajaba**
Shule ya Sekondari Nachingwea
SLP 80
Nachingwea

•••

Mhariri SautiElimu, Hongera kwa kuibua mjadala wa namna ya kuboresha elimu ya msingi nchini.
Kwa maoni yangu, elimu bora ni ile isiyo na ubaguzi. Ni elimu ambapo pia inamwezesha mwanafunzi kuwa mbunifu, mkosoaji panapostahili, huru na makini katika kutoa maoni yake.

Elimu tunayohita nchini ni ile inayompa fursa mwanafunzi kufahamu haki na majukumu yake katika jamii. Vile vile inamwezesha mtoto kupata ujuzi wa namna ya kuendesha maisha yake.

Kwa upande wa walimu, elimu bora ni ile inayompa mwalimu nafasi ya kutafakari na kuendelea kujifunza katika taaluma yake na kukubali kupokea maoni ya wanafunzi hata anapokosolewa.

**David Rainald**
Shule ya Sekondari Sabasaba
SLP 98
Mtwara

•••

Mhariri SautiElimu, Napenda kutoa ushauri wangu kuhusu elimu ya namna gani inayohitajika nchini.

Mara nyingi viongozi wanahimiza vijana kutosubiri ajira ya serikali na kutakiwa wajiajiri wenyewe. Hivi wanaposema vijana wajiajiri wana maana gani? Wamewaandaa vipi na katika nyanja zipi hadi waweze kujitegemea?

Elimu ya msingi ambayo ndiyo chanzo cha kujitegemea kwa kijana bado ni daraja tu la kuendelea na masomo ya juu. Kwa bahati mbaya, ni vijana wachache tu wanaopata nafasi ya kuendelea na masomo na wengi wanabaki kuwa kama wazamiaji waliotoswa ndani ya kina kirefu cha bahari na kukosa matumani ya kuokolewa.

Kwa kuzingatia wingi wa vijana wanaokosa nafasi ya kuendelea na elimu ya juu, nashauri somo la stadi za kazi liwe la vitendo zaidi na wanafunzi wafundishwe ufundi, kilimo, ufugaji na mbinu za kuendesha na kusimamia biashara. Fedha zinazotengwa na serikali kwa ajili ya somo hilo ziongezwe ili vifaa husika vinunuliwe.

Hayo yakitiliwa mkazo yatamkomboa kijana na kumwezesha kujitegemea.

**Patrick F. Malando**
SLP 993
Dodoma

# Vyanzo vya Taarifa


Je umeona mlolongo wa mabango ya HakiElimu? Mlolongo huo wa mabango 8 umegawanyika katika sehemu mbili. Mabango 4 yanahusu elimu bora na mengine 4 utawala wa elimu. Kila bango linauliza swali kuhusu elimu na kuna mchoro unaoendana na swali lililoulizwa.

Waweza kutumia mabango hayo kusisitiza masuala muhimu katika jumuiya yako. Kwa nini msikutane na kujadili maswali yaliyoulizwa katika mabango hayo? Tujulishe mliyojadili. Tungependa kusikia maoni yenu!




Mabango hayo yana rangi za kuvutia na ni makubwa ili kukuwezesha kuyabandika popote. Iwapo unahitaji mabango hayo tuandikie. Ukihitaji mabango ya ziada tufahamishe jinsi utakavyoyatumia.

HakiElimu Machapisho
Dar es Salaam




HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika elimu kwa kuwezesha jamii kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera za elimu, kuimarisha ubunifu wa uendeshaji wa mijadala na midahalo ya umma, kufanya utafiti yakinifu, wenye kuhoji, wenye kuchambua, kutetea na kushirikisha wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Shukurani kwa Shule za Msingi za Rung'abure (Serengeti) na Busagani (Ukerewe), Victor Simon na Goodluck Mashalla wa Mwanza.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yeyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala kwa HakiElimu.

ISSN 08568588
© HakiElimu, 2002

**Mhariri:** Rakesh Rajani
**Timu ya SautiElimu:** Mary Nsemwa, Lilian R. Kallaghe, Godfrey Telli na Kathy Relleen.
**Kutafsiri:** Lilian Kallaghe na Godfrey Telli
**Mchoraji:** Marco Tibasima

*Tuandikie!*
**HakiElimu, SautiElimu**
SLP 79401
Dar es Salaam
Simu: 022 2151852 / 3
Faksi: 022 2152449
Baruapepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

